East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 1, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo

*Dkt. Jackson Ndung'u Mwangi, PhD*[1]

[1] Chuo Kikuu cha KCA, S. L. P. 56808 - 00200, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-8791-4846; Barua pepe ya mawasiliano: jigmwas@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*24 Mei 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*TEKNOHAMA, Mtindo, Maudhui, Utandawazi.*

**IKISIRI**

Fasihi ni zao la jamii na hubadilika kila uchao. Uwakilishi wa suala la TEKNOHAMA katika tamthilia za kisasa umechukua mkondo mpya. Hii ni kwa sababu, kutokana na jinsi dunia inavyobadilika ndivyo masuala ya kiteknolojia pia yanavyoathiri fasihi ya sasa na kuipa mguso na taathira mpya. Licha ya uwakilishi wa TEKNOHAMA kuwa na umuhimu katika kukuza fani na maudhui katika fasihi, mchango wake katika tamthilia ya *Kigogo* haujafanyiwa utafiti, suala linalomchochea mtafiti kulitafiti. Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini mchango wa TEKNOHAMA katika kukuza maudhui katika tamthilia ya *Kigogo* ya Pauline Kea (2016). Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Uteuzi wa sampuli utafanywa kimakusudi na utafiti wenyewe ni wa muundo wa kiudhamano. Mtafiti atasoma makala mbali mbali kuhusiana na mada na kisha kuichanganua data kwa njia ya kimaelezo.

**APA CITATION**

Mwangi, J. N. (2022). Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 124-130. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671.

**CHICAGO CITATION**

Mwangi, Jackson Ndung'u. 2022. "Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 124-130. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671.

**HARVARD CITATION**

Mwangi, J. N. (2022) "Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 124-130. doi: 10.37284/jammk.5.1.671.

**IEEE CITATION**

J. N. Mwangi, "Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 124-130, May. 2022.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

**MLA CITATION**

Mwangi, Jackson Ndung'u. "Uhakiki wa Nafasi ya TEKNOHAMA katika Kukuza Maudhui katika Tamthilia ya Kigogo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, May. 2022, pp. 124-130, doi:10.37284/jammk.5.1.671.

## UTANGULIZI

Mtaalamu mmoja wa masuala ya mawasiliano, Kamau (2005) alidai kuwa dunia inaelekea kuwa ndogo kila uchao. Udogo huu unasababishwa na kuwepo kwa dhana ya usasa inayozaa dhana mpya ambayo ni teknolojia. Mrikaria (2007) anadai kuwa tunapozungumzia juu ya teknolojia, ni lazima tuhusishe suala la sayansi. Hivyo basi, sayansi na teknolojia ni vitu viwili vinavyokwenda sambamba na pamoja bila kuachana. Hii ni kwa sababu, teknolojia ni maendeleo ya kisayansi katika hatua mbali mbali za uvumbuzi wa mwanadamu. Kwa mujibu wa utafiti huu, teknolojia ya habari na mawasiliano ni zao la teknolojia mpya ambayo hukuzwa kutokana na uvumbuzi wa kiteknolojia. Ulimwengu wa sasa na utandawazi umesababisha kuzagaa kwa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) hususan kompyuta na vitumi vyake. Kwa hivyo, maendeleo ya sayansi na teknolojia na uhusishaji wake katika fasihi ya sasa yamesababisha fasihi kukua na kuipa mguso mpya kwa msomaji.

Ishara muhimu ya utandawazi ni ule uwezo wa kuyagusa maisha ya wanajamii wengi kwenye jamii anuwai katika nyanja mbali mbali za elimu, uchumi, siasa na utamaduni kwa jumla. Kwa vile fasihi ni zao la jamii, ina uwezo wa kukua jinsi mwanadamu anavyokuwa. Alomo (2016) anadokeza kuwa uwakilishaji wa teknolojia mpya katika kazi ya fasihi huipa fasihi mguso na taathira ya kipekee kwa vile huhusisha vipengele vya kisasa katika fasihi. Anaendelea kudokeza kuwa uvumbuzi wa vyombo vya mawasiliano na habari vimesaidia sana katika kukuza na kuendeleza fasihi ya leo. Gikambi (2015) katika tasnifu yake anadokeza uhusishi wa masuala ya teknolojia na utandawazi katika fasihi yana jukumu la kipekee katika kukuza na kuendeleza dhamira pamoja na maudhui anuwai katika kazi husika ya kifasihi.

Kwa mujibu wa utafiti huu, ni wazi kuwa TEKNOHAMA ina jukumu la kipekee katika fasihi hususan inayotungwa na watunzi wa kisasa. Watunzi hawa wanahusisha vyombo anuwai vya habari kama vile runinga, redio, gazeti, tarakilishi na mitandao ya kijamii katika kuwakilisha maudhui ili kuipa kazi ya fasihi mguso mpya. Kuhusisha vipengele hivi vya teknolojia ya habari vinadhihirisha wazi kuwa fasihi kama ilivyo jamii inakuwa na kuenea katika taasisi mbalimbali zinazohusishwa na mwanadamu. Vile vile, vyombo hivi vina jukumu la kipekee katika kuipitisha na kuieneza fasihi kwa wanajamii kwa njia rahisi na mwafaka. Hii ni kwa sababu wanadamu wa sasa wana ari ya kujinasibisha na masuala mapya yanayovumbuliwa na kubainika katika jamii. Utafiti huu ulinuia kubainisha ni kwa kiwango kipi mtunzi wa tamthilia ya *Kigogo* amefanikiwa kutumia vipengele vya TEKNOHAMA katika kazi yake na mchango wake katika kukuza maudhui katika tamthilia husika.

## MSINGI WA NADHARIA

Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya19 na kufafanuliwa zaidi na Goffman (1952) aliyeishi kati ya mwaka (1922-1982). Baadhi ya wataalamu wengine waliotoa mchango wao ni Gustav (1850), Lukacs (1979),Wellek (1960), Arthur (1918) na Hegel (1971). Lukacs (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko ya mabadiliko yaliyopo. Uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi kuhusu uhalisia. Naye Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waandishi wa kazi teule wanatoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira.

Utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

- Kazi ya fasihi inajitosheleza. Tamthilia ni kazi ya sanaa kwa vile ina msuko, mtindo, wahusika na ujumbe. Mhimili huu ulitusaidia kuonyesha kuwa tamthilia teule ni kazi ambayo inajitosheleza kama kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu ina sura, ploti, maudhui, wahusika na zinatumia mitindo ya kisanii.

- Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi kupitia kwa wahusika. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti katika uchanganuzi wa maudhui yanayodokezwa na TEKNOHAMA katika tamthilia yaliyo ya kikweli katika jamii ya sasa.

- Msanii anaangalia hali mbalimbali za uhalisia zinazojitokeza katika kazi ya fasihi na kuchunguza chanzo chake, mazingira pamoja na mpito wake kiwakati. Isitoshe, mwanasanaa Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi fulani cha historia na kuyatumia kuwasawiri wahusika, dhamira na hata maudhui katika kazi husika.

## NAFASI YA TEKNOHAMA KATIKA KUWASILISHA MAUDHUI MBALIMBALI KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

Kwa mujibu wa utafiti huu, ni bayana kuwa TEKNOHAMA inatekeleza majukumu ya kipekee katika kukuza na kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Kigogo***.** Vipengele vya TEKNOHAMA vinavyotumiwa na mtunzi wa tamthilia hii ni kama vile televisheni, redio, gazeti, simu za rununu na mitandao ya kijamii. Isitoshe, mtunzi anaonekana akitumia vyombo hivi vya habari kukuza na kubainisha maudhui mbali mbali kama vile, uzalendo, maandamano na migomo, ukombozi, ukoloni, uongozi mbaya, vifo na ufisadi. Mtafiti amebaini kuwa uhusishaji wa vyombo vya habari katika tamthilia hii teule una jukumu la kipekee katika kukuza maudhui na kuifanya tamthilia yenyewe kuwa na mguso wa kisasa. Hii ni kwa sababu, msomaji wa tamthilia yenyewe ana nafasi ya kujinasibisha na masuala pamoja na vyombo vya kiteknolojia anayokumbana nayo kila uchao.

### Uzalendo

Mojawapo ya maudhui muhimu yanayokuzwa na kuendelezwa na vyombo vya habari ni uzalendo. Katika ukurasa wa nne, mjumbe kupitia kwa redio anatangaza kuwa kutakuwepo na kusherehekea kwa siku ya uhuru ili kuwakumbuka vigogo wa jimbo la Sagamoyo waliopigania uhuru wa jimbo hili ili kulikomboa kutokana na wakoloni. Isitoshe, mjumbe anadokeza kuwa ili kuonyesha uzalendo wa nchi yao, ilikuwa ni vyema sherehe hizi za uhuru kufanywa mwezi mzima mtawalia.

> *Yafuatayo ni matangazo maalum. Wananchi watukufu wa Jimbo la Sagamoyo mnatangaziwa kuwa kipindi cha mwezi mzima wa kusherehekea uhuru wetu kitaanza kesho. Katika kipindi hiki adhimu, mnatakikana kuwakumbuka majagina wetu wa uhuru; waliopigana ili kutunasua kutoka kwenye silisili za utumwa (Uk. 4).*

Akiwa kwenye ikulu, Mzee Marara (Majoka) alitangaza kuwa si jambo ndogo kusherehekea miaka sitini ya uhuru tangia Wanasagamoyo walipojikomboa kutoka kwenye minyororo ya utumwa. Sababu ya Majoka kusema haya ilikuwa ni kuwarai wananchi wa jimbo la Sagamoyo kuonyesha kuwa kwa kweli walilienzi jimbo lao na waliwadhamini wachache waliojitolea mhanga ili kupigania uhuru wa nchi yao.

> *Ndugu zangu Wanasagamoyo, kuisheherekea miaka sitini baada ya kujikomboa kutoka kwenye mikatale ya utumwa si jambo ndogo. Ninawashauri nyote muwakumbuke sana waliojitolea mhanga, wakahatarisha maisha yao na hata kufa ili tuyavune matunda haya ya uhuru. Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba za kikoloni kuturejesha kwenye utumwa wa kimawazo au wa namna yoyote (Uk 5).*

Mifano hii inaonyesha kuwa wananchi wa Sagamoyo wakiongozwa na viongozi wao walidhamini sana nchi yao na walikuwa na ari ya kuonyesha uzalendo kwa nchi hii na hata kwa viongozi waliopigania uhuru wa nchi yao. Dhana hii ya uzalendo inakuzwa na kuendelezwa kupitia vyombo vya habari ( redio) katika jimbo hili.

Katika jimbo hili la Sagamoyo, vyombo vya habari vinaendelea kukuza dhana ya uzalendo hususan

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

kutokana na wafadhili wanaodhamini vyombo vya habari vinavyoendeleza na kufanikisha juhudi za wazalendo kama Tunu kuleta mabadiliko miongoni mwa wanajamii. Katika ukurasa wa 33, Majoka anasema kuwa

> *"Na hawa wafadhili wao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo Twajiweza."*

Isitoshe, inabainika kuwa ili kupigania juhudi za kizalendo, ilikuwa ni sharti wazinduzi kama Tunu na Sudi wapate ufadhili wa kifedha ili kuendeleza shughuli zao za kizalendo. Majoka anaonekana akiudhika sana hususan anapogundua kuwa kuna wafadhili wa kigeni wanaofadhili gazeti ili wazalendo hawa waendeleze juhudi zao za kuikomboa Sagamoyo.

> ***Majoka:*** *Wafadhili wa gazeti ni akina nani?*

> ***Kenga:*** *Ni hao hao wafadhili wake. Na kwamba ngoma huvutia wapi?*

Kupitia kwa vyombo vya habari kama vile Gazeti za Mzalendo, wananchi wanatoa maoni yao kuhusu kiongozi mzalendo wanayempenda. Katika ukurasa wa 33, wananchi wanatoa maoni yao na kuonyesha kuwa wanampenda sana Tunu kutokana na juhudi zake za ukombozi zinazonuia kuleta mabadiliko maishani mwao.

> ***Majoka****: Huoni watu wakitoa maoni yao hata eti Tunu awanie uongozi wa Sagamoyo?*

> ***Kenga:*** *(Kwa mshangao huku akizidi kulikodolea macho Gazeti) Mama wee! Sikuwa nimeyasoma haya, Eti asilimia zaidi ya sitini iko tayari kumpigia kura ikiwa atasimama?( Akitingisha kichwa) siamini! Nafikiri walitilia chumvi. Tunu hawezi kupigiwa kura hata!)*

Mifano hii inadhihirisha kwa uwazi kuwa vyombo vya habari kama vile redio, gazeti na runinga viko katika mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wananchi wa jimbo la Sagamoyo wako tayari kuendeleza na kukuza uzalendo.

## Maandamano na Migomo

Vyombo vya habari viko katika mstari wa mbele kuendeleza na kukuza maudhui ya migomo na maandamano katika tamthilia hii ya *Kigogo*. Inabainika kuwa wafanyikazi wanagoma kutokana na mazingira mabovu ya kufanyia kazi pamoja na kulipwa mishahara ambayo kwa kawaida inakuwa vigumu kuyakidhi mahitaji yao ya kila siku. Katika ukurasa wa 31, Kenga anamuonyesha Majoka habari za migomo na maandamano kutoka kwenye gazeti. Vyombo vya habari vikiwemo gazeti vinatekeleza majukumu muhimu ya kuwajuza na kuwafahamisha Wanasagamoyo kuhusiana na madhila wanayopitia wafanyikazi kutokana na uongozi mbaya unaoendeshwa na Majoka akishirikiana na vibaraka wake. Baada ya vyombo hivi kuweka wazi dhuluma ambazo wafanyikazi wanapitia, vinawaonyesha wafanyikazi wakigoma na kuandamana wakiwa na nia ya kudai haki kutokana na dhuluma wanazozipitia.

> ***Kenga****: Tazama picha hizi za waandamanaji.*

> ***Majoka:*** *(Akilikodolea macho gazeti) Salaale! Kwani wanaandama kila siku?*

Juhudi za gazeti hili kuwapasha wananchi habari kuhusiana na suala la migomo linauweka uongozi wa Majoka katika hali mbaya na kumfanya ajawe na wasiwasi. Isitoshe, gazeti lenyewe linaweka wazi uongozi mbaya ulioendelezwa na Majoka. Vilevile, Gazeti hili linaonyesha maandamano yanayoendelea kila siku kudhihirisha kuwa Wanasagamoyo hawako radhi kulegeza kamba katika juhudi za kutafuta haki na usawa katika jamii.

Katika ukurasa wa 37 na 38. *Runinga ya Mzalendo* inapeperusha moja kwa moja *(live coverage)* jinsi Tunu na wenzako wanavyoongoza maandamano. Majoka anaona kuwa maandamano haya ni hatari mno katika jimbo hili kwani yanautia tope uongozi wake. kuonyeshwa kwa maandamano haya moja kwa moja yanamfanya Majoka kuibuka na mbinu ya kutaka kuwaondoa na kuwaua viongozi wa maandamano haya ambao ni akina Tunu na Sudi.

> ***Kenga:*** *Hata hawana haya: Live coverage?*

> ***Majoka****: Maandamano haya yanazidi kutuharibia sherehe yetu.*

> ***Kenga****: Tuichukulie Hatua Runinga ya Mzalendo, siipendi hii mitandao ya kijamii.*

Katika kuonyesha maandamano haya moja kwa moja, runinga hii inatekeleza jukumu la kipekee la kuukosoa uongozi dhalimu unaoendelezwa na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

Majoka. Isitoshe, inaonyesha jinsi hali za wafanyikazi zilivyo duni na matatizo wanayoyapitia kutokana na uongozi wa kidikteta ulioongozwa na Majoka. Mitandoa ya kijamii pia inapeperusha maandamano na migomo moja kwa moja kupitia kwa simu na tarakilishi. Suala hili linamtia kiwewe sana Majoka kuwa watu wengi wakiwemo vijana wanapa uwezo wa kutambua maovu yanayotekelezwa na Majoka na uongozi wake.

**Ukombozi**

Katika jimbo la Sagamoyo, kuna wahusika wanaojitolea mhanga ili kuleta mabadiliko miongoni mwa wananjamii. Wanaoongoza harakati za kuleta mabadiliko ni Tunu na Sudi ambao baadaye wanapata wafuasi wengine kama vile Ashua, Kenga na Kingi, Chopi na Mama Pima. Tunu na Sudi wanapojaribu kuleta mabadiliko katika jamii na kuamua kuongoza maandamano kupinga uongozi dhalimu wa Majoka, matendo yao yanapeperushwa katika vyombo vya habari. Katika ukurasa wa 32 tunamuona Kenga akimwonyesha Majoka picha kutoka kwenye gazeti Tunu na Sudi wakiongoza maandamano.

> ***Kenga****: (Akifungua ukurasa mwingine) Tazama picha hizi nyingine.*
>
> ***Majoka:*** *(Kwa mshangao) Ala! Tunu aliongoza maandamano? (Kimya huku akiangalia kwa makini zaidi picha kwenye gazeti.) Tena aliandamana na hawa wanaojiita wanaharakati!*

Kuonyeshwa kwa picha hizi na Gazeti hili kunawapa watu matumaini kwa kuonyesha kuwa kuna watu wanaojitolea mhanga katika kujaribu kutafuta suluhu ya madhila wanayopitia Wanasagamoyo. Isitoshe, gazeti hili linawapa wakombozi matumaini kwani nia zao za kuleta mabadiliko katika jamii zinatambuliwa na kuwekwa wazi.

Katika ukurasa wa 37, juhudi za Tunu kuleta mabadiliko katika jamii zinadhihirika. Mitandao ya kijamii inapeperusha picha za moja kwa moja kutoka Runinga ya Mzalendo zikimuonyesha akiwahutubia watu katika soko la Chapakazi. Suala hili linamfanya Majoka na Kenga kuudhika sana na kuamua kuifunga runinga ya Mzalendo. Suala hili linaonyesha wazi kuwa mitandao ya kijamii na Runinga kama vile Runinga ya Mzalendo zinafanikisha suala la ukombozi kwa kuunga mkono juhudi za Tunu za kuhakikisha kuwa kuna mabadiliko katika jamii.

> ***Kenga:*** *(Akionyesha simu yake) Ona habari hizi kwenye mtandao wa kijamii. Nimeambiwa kuwa zinapeperushwa moja kwa moja katika Runinga ya Mzalendo,*
>
> ***Majoka****: (akitazama yaliyo kwenye rununu ya Kenga.) Lo! Kwani wameanza tena? Tunu anacheza na simba anayenyonyesha.*
>
> ***Kenga****: Naona watu wengi wa sokoni hapo. Na huyu aliye kando si ni…*

Katika ukurasa wa 38, tunayaona maandamano yakionyeshwa moja kwa moja (Live Coverage) kwenye Runinga ya Mzalendo. Majoka anasema kuwa maandamano haya yanamharibia uongozi wake na pia yanatia doa maandalizi ya sherehe ya kufurahia siku ya uhuru.

> ***Kenga:*** *Hata hawana haya. Live Coverage?*
>
> ***Majoka:*** *Maandamano haya yanazidi kutuharibia sherehe yetu.*

Ni dhahiri kuwa kwa kweli, vyombo vya habari vinachukua nafasi muhimu katika kuangazia suala la ukombozi katika jamii. Ikumbukwe kuwa vyombo hivi vinamsawiri mwanamke (Tunu) kama kigezo muhimu katika kuendeleza harakati za ukombozi.

Isitoshe, katika ukurasa wa 38, vyombo vya habari vinaonekana vikimuunga mkono Tunu vinapodai kuwa asilimia 60 ya wananchi wa jimbo la Sagamoyo wako tayari kumpigia kura Tunu hata kama alikuwa mwanamke. Ukweli ni kwamba, juhudi za vyombo hivi vya habari zinazaa matunda kwani tamthilia hii inapofikia kikomo, Wanasagamoyo wanaungana pamoja na kuhudhuria mkutano waTunu na baadaye anachaguliwa kuwa kiongozi wa Sagamoyo.

**Ufisadi**

Vyombo vya habari katika jamii hii vinasawiri suala la ufisadi lililokidhiri sana katika jimbo hili la Sagamoyo. Katika ukurasa wa 32, tunaona gazeti likionyesha jinsi uongozi wa Majoka ulivyojaa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

ufisadi na matumizi mabaya ya mali ya umma. Gazeti hili linaonyesha jinsi pesa zilizokusanywa katika Soko la Chapakazi zilivyovujwa. Pia, inaeleza kuwa Majoka ananuia kulifunga Soko la Chapakazi ndiposa aweze kuinyakua ardhi ile na kujenga hoteli ya kifahari akiwa na nia ya kujinufaisha mwenyewe. Uvumbuzi huu unamtia kiwewe sana Majoka na kumwacha akiwa amejawa na huzuni isiyokuwa na kifani.

**Uongozi Mbaya**

Katika tamthilia ya *Kigogo*, vyombo vya habari vinasawiri jinsi viongozi wanavyoendeleza uongozi mbaya na kusababisha kilio pamoja na maafa mengi katika jamii. Katika ukurasa wa 38, kupitia kwenye gazeti na runinga, tunawaona polisi wakiwatawanya wananchi waliokuwa wakiandamana kwa amani. Majoka anamwambia Kenga kikosi cha polisi kikiongozwa na Chopi kimefanya kazi nzuri. Jambo hili linadhihirisha wazi kuwa amri ya kuwafanya polisi kutumia nguvu kwa waandamanaji waliokuwa wakiandamana kwa amani ilitoka kwa Majoka, jambo linalodhihirisha uongozi mbaya.

Vyombo vya habari kama vile gazeti vinaonyesha jinsi soko la Chapakazi lilivyokuwa chafu licha ya kuwa wafanyibiashara kama vile Boza, Kombe na Sudi walitozwa kodi ya kulinadhifisha soko lile. Vile vile, gazeti linaweka wazi mpango wa Majoka wa kutaka kulifunga soko la Chapakazi akiwa na nia ya kujenga hoteli ya kifahari kwa manufaa yake mwenyewe. Katika ukurasa wa nne, tunamwona mjumbe kupitia redio akitangaza Majoka alikuwa ametoa amri kuwa ni lazima Wanasagamoyo wangesherehekea siku ya uhuru kwa mwezi mzima mtawalia. Hii ni ishara ya uongozi mbaya kwani ilikuwa ni hila tu ya kuwapumbaza Wanasagamoyo kwa nia ya kujinufaisha yeye mwenyewe na aila yake.

Majoka anapogundua kuwa vyombo vya habari havimuungi mkono ila vinampigia upato Tunu, anaonekana akiibuka na wazo la kutaka kukandamiza vyombo vya habari ambavyo havimuungi mkono. Anadai kuwa kwa vile *Runinga ya Mzalendo* inapeperusha habari kuhusu maandamano yanayoongozwa na Tunu, anaamua kuifunga na kuachwa na kituo kimoja tu cha kutangazia habari kiitwacho *Sauti ya Mashujaa*. Mifano hii ni idhibati kamili kuwa vyombo vya habari vilikuwa mstari wa mbele kuweka wazi uongozi mbaya uliokuwa ukitekelezwa na Majoka na kuwapigia upato viongozi walioonyesha nia ya kuleta mabadiliko katika jamii kama vile Tunu na Sudi.

**Maudhui ya Ukoloni**

Kwa mujibu wa utafiti huu, vyombo vya habari vinaibua suala ya ukoloni. Kuna aina mbili kuu za ukoloni unaobainika katika tamthilia hii. Kuna ukoloni mkongwe uliobainishwa na wakoloni wageni/wazungu waliofika katika mji wa Sagamoyo na kuanza kuwanyanyasa na kuwadhulumu. Ili kujiondoa kwenye minyororo ya wakoloni hawa, iliwabidi viongozi wa jimbo la Sagamoyo wajitolee mhanga na hata wengine kufa ili waweze kuwafukuza wakoloni hawa. Juhudi za Wanasagamoyo kujaribu kujikomboa zinabainishwa na vyombo vya habari wakati mjumbe anapotoa matangazo yake kupitia redio. Anasema:

> *Katika kipindi hiki adimu, mnatakikana kuwakumbuka majagina wetu wa uhuru; waliopigana ili kutunasua kutoka kwenye silisili za utumwa (Uk. 4).*

Inadaiwa kuwa majagina hawa walijitolea kwa udi na uvumba wakiwa na nia ya kuitafutia nchi yao uhuru.

Sababu ya Wanasagamoyo kusherehekea uhuru ni kutokana na juhudi za wakombozi na wapenzi wa nchi waliopigania uhuru wa watu wao kutoka kwenye minyororo ya wakoloni. Mjumbe anaendelea kusema kuwa:

> *Ninawashauri nyote muwakumbuke sana waliojitolea mhanga, wakahatarisha maisha yao na hata kufa ili tujivunie matunda haya ya uhuru (Uk. 4).*

Katika kuangazia suala la ukoloni mambo leo, viongozi wa Kiafrika waliochukua hatamu za uongozi walionekana wakiendeleza kaida za kikoloni na kuanza kuwadhulumu Waafrika wenzao. Majoka anapochukua uongozi wa Jimbo la Sagamoyo, vyombo vya habari vinaweka wazi suala la dhuluma na unyanyasaji unaoendelezwa na kiongozi huyu. Tunaona *live coverage* ya wafanyikazi wakigoma kwa kutolipwa mishahara

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.671

na pia kutokana na hali duni za kufanyia kazi. Isitoshe, gazeti linabainisha mpango wa Majoka wa kuwafurusha watu kutoka kwenye soko la Chapakazi, kuinyakua ardhi ile na kutaka kujijengea hoteli ya kifahari. Mifano hii ni dhibitisho tosha kuwa kwa kweli vyombo vya habari vinachukua nafasi muhimu kuangazia suala la ukoloni ambao unabainika kuwa ulikuwa kero kwa wanajamii wa Sagamoyo.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu umebaini kuwa kwa kweli, fasihi hukua kama ilivyo jamii huku. Siku za hivi karibuni, kumekuwepo na uvumbuzi wa kiteknolojia na kisayansi ambao umeathiri takriban nyanja zote za maisha ya mwanadamu pamoja na taasisi na taaluma mbalimbali ikiwemo fasihi. Katika nyanja ya habari na mawasiliano, suala la uhusishi wa teknolojia limekuwa bayana sana hadi kukazuka taaluma ya teknolojia ya habari na mawasiliano almaarufu TEKNOHAMA. Kwa kurejelea tamthilia ya *Kigogo*, mtunzi Pauline Kea amebainika kuhusisha suala hili katika utunzi wake na kuipa kazi yake athari na mguso wa kisasa. Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kuwa mtunzi wa tamthilia ya *Kigogo* amefanikiwa sana katika kuhusisha vipengele mbali mbali vya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kukuza dhamira na maudhui katika kazi yake. Maudhui kama vile uzalendo, maandamano na migomo, ukombozi, ufisadi, uongozi mbaya na ukoloni yamedokezwa na kufafanuliwa kupitia vipengele anuwai vya teknolojia ya habari kama vile mitandao ya kijamii, redio, runinga na hata magazeti. Dhana za kisasa kama vile mitandao ya kijamii na *live coverage* zimetumiwa na mwandishi katika kufanikisha maudhui yake. Uhusishi wa TEKNOHAMA katika kufanikisha maudhui katika tamthilia hii pia unatekeleza majukumu anuwai kama vile, kuipa kazi ya fasihi mguso wa kisasa na kumfanya msomaji kutangamana na masuala mapya ambayo yanaibuka katika taaluma ya mawasiliano na habari kama vile mitandao ya kijamii. Watafiti wanapendekeza kuwa tafiti za baadaye zifanywe ili kubaini mchango wa TEKNOHAMA katika ukuaji wa na ustawishaji wa Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika kote duniani.

## MAREJELEO


Alomo, O. S. (2016) Uwakilishi wa Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili iliyoandikwa na Said, A. Mohamed na Wadi, K. Wamitila. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Egerton.

Gikambi, P. H. (2015) Teknolojia ya Kiswahili katika Utafiti wa Kiswahili: Kifani cha mradi Salama. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kamau, S. N. (2005) Matumizi *ya Kiswahili katika Tarakilishi*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kea, P. (2016) *Kigogo.* Story Moja Publishers. Nairobi, Kenya.

Leech, G. na Short, M. (1981) Style in Fiction. A Linguistic Introduction to English Fiction Prose. England: Longman Group Limited.

Leech, G. (1969) *A linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group. Lodge, D. (1972) *Mh 20th Century Literary Criticism*. London: Longman Group.

Lodge, D. (1972) *Mh 20th Century Literary Criticism*. London: Longman Group.

Lukacs, G. (1963) *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Publishers.

Moureen, N. M. (2015) Masuala Ibuka katika Riwaya za Kisasa: Kidagaa Kimemwozea na Mhanga wa Nafsi Yangu. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mrikaria, E. S. (2007) *Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya*. Swahili Forum 14 (2007) :197-206Wales, K. (1991) *Dictionary of stylistics.* New York: London Group.

Wellek, R. na Werren, A. (1973) *Theory of Literature*. Harmondswort: Penguin Books Limited.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.